

JINA: \_\_\_\_\_  
NAMBARI YA MTAHINIWA: \_\_\_\_\_  
DARASA: \_\_\_\_\_  
SAHIHI: \_\_\_\_\_  
TAREHE: \_\_\_\_\_

1013/1

P1 KISWAHILI

KARATASI 1

MWIGO

MECHI / APRILI 2018

MUDA: SAA 2

**MTIHANI WA MWIGO  
KARATASI YA KWANZA  
MUDA: SAA 2**

**MAAGIZO**

1. Andika jina lako na namba yako kwenye nafasi ulizoachiwa..
2. Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa.
3. Mtihani huu una sehemu **Nne kuu: Insha, Ufahamu, Matumizi ya lugha na sajili ya Lugha.**
4. Ni muhimu sana ufuate maagizo ulipewa mwanzoni mwa kila sehemu.
5. Andika majibu yako kwenye nafasi ulizoachiwa.
6. Usitoe kratasi yoyote katika kijitabu hiki.
7. **Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.**

**KWA MATUMIZI YA MTAHINIWA PEKEE**

SEHEMU	SWALI	UPEO	ALAMA
1	1	20	
2	2	20	
3	3	30	
	4	20	
4	5	10	
<b>JUMLA</b>			

Kijitabu hiki kina kuras 16 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

## **SEHEMU YA KWANZA: INSHA (ALAMA 20)**

1. Andika insha isiyopungua maneno 350 kuhusu mojawapo ya mada zifuatazo:
  - a) Mitandao ya kijamii imeleta mabadiliko makubwa maishani. Jadili
  - b) Chuoni mwenu mna hafla ya mahafali. Andaa ratiba ya matukio itakayofuatwa.
  - c) Maskini haokoti, akiokota huambiwa kaiba.
  - d) Andika insha itakayoanza kwa: “Jua lilikuwa tayari limeshatua na kupisha giza kushika hatamu..... Endelea.”

## **2. SEHEMU YA PILI: UFAHAMU (ALAMA 20)**

*Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali*

Baa la njaa si jambo geni katika ukanda huu wetu wa Africa na hasa sehemu za kaskazini mwa jangwa la sahara. Baa hili limekuwepo tangu jadi za fadi, na kama lingetwa mgeni, basi ni wa mara kwa mara. Nchini Kenya, kwa mfano, baa hili limekuwepo baada ya kipindi cha misimu kadhaa au miaka kadhaa.

Swali tunalopaswa kujiuliza ni kwa nini baa hili katika jaribu hizi zetu? Majibu ni mengi, lakini la kushangaza ni kuwa pamoja na majaribu yote hayo halitapatikana suluhu la kudumu.

Wengi husema kuwa baa la njaa nchini Kenya lina usuli wake katika historia ya utawala. Ambapo wakati wa enzi za ukoloni ardhi yote yenye rutuba ilinyakuliwa na mabeberu. Ardhi hiyo ilitumiwa kwa ajili ya kukuza mazao ya kibashara kama vile kahawa na chai. Mwfrika aliwachiwa sehemu ambazo hazikuwa na ruttuba wala maji. Ukame nao ni sababu nyengine ya njaa. Lakini la kushangaa ni kuwa mvua nyingi au mafuriko pia ni kizungumkuti huku kwetu Kenya. Tufikirie kwa mfano mvua za ‘elnino’ ambapo kutokana na mafuriko mimea yote ilisombwa na maji na kuwaacha watu na mashamba meupe.

Suluhu la baa hili litatokana na sisi wenyewe wakenya; raia pamoja na serekali. Ni muhimu kwa nfano watu kujizoesha kula vyakula anuwai kuliko kutengemea mahindi peke yake. Vyakula vya kiasili kama vile mihogo, ndizi za kisukari, nduma, viazi na kadhalika vinaweza kukuzwa katika maeneo mengi nchini na vinatoa lishe bora. Hali kadhalika wakulima watumie teknolojia ya sasa ya ukusaji mimea, ambayo itawawezesha kupata mazao bora na mengi. Mbinu mpya za unyunyiziaji mashamba ni mfano kabambe. Serekali kwa upande mwingine ina jukumu nyeti la kuhakikisha kuwa miundo msingi imeimarishwa hasa katika sehemu za mashambani ili kuwezesha ukulima. Mbinu za usafiri, usambazaji wa mali na nguvu za umeme ni mifano bora. Jambo hili litawahimiza wakulima, na pia wale walio mjini watapata ile hamu ya kurudi mashambani na kushughulikia kilimo.

Aidha serikali iweke sera katika sekta ya kilimo. Ambapo wakulima watapata malipo mazuri kwa mazao yao. Sera za ugawaji ardhi pia ziwekwe, ili watu wenye madalbasari ya mashamba na viunga vikubwa vikubwa nya mimea isyotunzwa washauriwe kulima au kuwapa watu wengine walime.

Kilimo ndicho uti wa mgogo wa taifa letu na kisipotiliwa makazo, hakuna ufanisi wowote utakaofikiwa. Watu wenyenjaa hawawezi kusikilizana sembuse kushirikiana katika miradi ya mandeleo!

### **MASWALI**

- a) Taja kichwa mwafaka kwa taarifa hii (alama 1)
- 
- 

- b) Kwa mujibu wa taarifa hii, eleza sababu zinazosababisha baa la njaa nchini Kenya. (alama 4)

- c) Pendekeza njia zozote tano za kuzuia njaa nchini. (alama 5)

- d) Kwa maoni yako, eleza jinsi wanafunzi kutika vyuo vya walimu wanavyoweza kuchangia njaa nchini Kenya (alama 5)

- e) Eleza athari za baa la njaa kwa nchi. (alama 3)

- f) Eleza maana ya maneno haya kwa mujibu wa taarifa (alama 2)
- (i) Anuwai
- 
- 
- 
- 

- (ii) Viunga
- 
- 
- 
- 

### **3. SEHEMU YA TATU: MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 50)**

*Jibu maswali yote katika sehemu hii.*

- a. Andika maana mbili za sentensi hii:

- Mtu mwenye kofia ni jirani yangu. (alama 2)
- 
-

- 
- 
- b. Tambulisha viambishi na mzizi katika neno:

Wanakaa

(alama 2)

---

---

---

- c. Andika kwa wingi.

Ua huu mrefu unaizingira nyumba.

(alama 2)

---

---

---

- d. Andika kwa kufuata maagizo:

Nani amezipoteza funguo zako? Anza: Funguo..

(alama 2)

---

---

---

- e. Tumia – baya – kama kivumishi katika sentensi.

(alama 2)

---

---

---

- f. Onyesha kundi Nomino na kundi Tenzi katika sentensi ifuatayo:

Alivumilia mpaka mwisho

(alama 2)

---

---

- 
- 
- 
- 
- 
- g. Andika sentensi moja ili kuonyeasha matumizi ya hali isiyodhihirika. (alama 2)

---

---

---

---

- h. Kanusha sentensi ifuatayo.

Mchezo utakapokuwa ukiendelea, mashabiki watakuwa wakishangilia (alama 2)

---

---

---

---

- i. Bainisha kitenzi katika sentensi ifuatayo na ueleze ni cha aina gani.

Yule ndiye mwenye matunda haya. (alama 2)

---

---

---

---

- j. Tunga sentensi yenye muundo ufuatao

W+ T +H + N (alama 2)

---

---

---

---

- k. Sentensi ifuatayo ni ya aina gani?

Kijana njoo (alama 1)

---

---

- l. Andika kiunganishi kinachoonyesha majuto

(alama 1)

---

---

---

m. Kwa kutoa mifano, eleza miundo miwili ya silabi. (alama 2)

n. Andika kifungu kifuatacho katika usemi halisi.

Karema alimsihi mama yake amruhusu kwanza adurusu masomo yake halafu ajifulie  
nguo. Mama yake alimpa saa moja. (alama 4)

---

---

---

o. Taja nomino za jamii za maneno yafuatayo:

Ndizi

---

Kuni (alama 2)

---

#### 4. MATUMIZI YA LUGHA

A. Andkia jibu la salamu hii: alamsiki (alama 2)

---

---

---

B. Tegua kitendawili hiki: Mbona mwaandamana hata na kina babu na mizigo, safari ya wapi?

---

---

---

C. Methali ifuatayo inatoa ushauri gani? (alama 2)  
Kumcha Mungu si kilemba cheupe

- 
- 
- 
- D. Godoro ni kwa kitanda na zulia ni kwa (alama 1)
- 
- E. Anapofungiwa mshukiwa huitwa (alama 1)
- 
- F. Watu hawa hufanya kazi gani? (alama 2)
- i) Mnyapara
- 
- ii) Sarahangi
- 
- 
- G. Kapu la kubebbea matunda huitwa (alama 2)
- 
- 
- H. Sikio ni kwa kusikiliza, figo ni kwa (alama 1)
- 
- I. \_\_\_\_\_ ni aina ya ndege ambaye hunyakua vifaranga (alama 1)
- J. Sehemu kubwa ya bahari iliyoingia ndani ya pwani huitwa (alama 1)
- 
- K. Pambo ambalo huvaliwa kwenye uti wa pua huitwa (alama 1)
- 
- L. Andika kisawe cha:
- i) Kabumbu

---

---

ii) Mwanasesere

(alama 2)

---

---

M. Bunda ni kwa karatasi, kicha ni kwa \_\_\_\_\_ ilhali \_\_\_\_\_  
ni kwa nzige (alama 2)

## 5. SEHEMU YA NNE: SAJILI YA LUGHA (ALAMA 10)

Huku ukitoa mifano, eleza sifa za kimsingi zinazotambulisha sajili ya mazungumzo ya kawaida

(alama 10)